


Khalai azungumza na mimea


-  Ursula Nafula
-  Jesse Pietersen
-  Ursula Nafula
-  Kiswahili
-  Level 2

(imageless edition)







Khalai ni msichana mwenye umri wa miaka saba. Jina lake lina maana ya 'aliye mzuri' katika lugha yake ya Lubukusu.




Khalai anaamka na kuongea na
mmea mchanga wa Mchungwa,
“Tafadhali mti wa Mchungwa, kua
mkubwa uzae machungwa mengi
mabivu.”




Khalai anaenda shuleni na njiani
anaongea na Nyasi, "Tafadhali
Nyasi, kua kijani zaidi na zaidi na
wala usikauke."




Khalai anayapita Maua ya mwituni
na kusema, “Tafadhali Maua,
endelea kunawiri ili niweze
kukuweka kwenye nywele zangu.”




Akiwa shuleni, Khalai
anazunguumza na Mti ulioko
katikati ya shule, “Tafadhali Mti,
toa matawi makubwa ili tusome
chini ya kivuli chako.”



Khalai anazunguumza na ua unaoizingira shule yake, “Tafadhali ua, kuwa mwenye nguvu ili uzuie shule yetu kutokana na watu wabaya.”



Anaporudi nyumbani alasiri, Khalai
anautembelea mti wa Mchungwa
kuangalia kama machungwa
yameiva.



“Machungwa bado mabichi,”
Khalai anashusha pumzi.

“Nitakuona kesho, we mti wa
machungwa. Labda utanipa
chungwa bivu wakati huo.”



Storybooks Canada

storybookscanada.ca

Khalai azungumza na mimea

Written by: Ursula Nafula

Illustrated by: Jesse Pietersen

Translated by: Ursula Nafula

This story originates from the African Storybook (africanstorybook.org) and is brought to you by Storybooks Canada in an effort to provide children's stories in Canada's many languages.



This work is licensed under a Creative Commons
[Attribution 4.0 International License](http://creativecommons.org/licenses/by/4.0/).